

# MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

Simu: +255-26-2963888,  
0800 110063  
Barua Pepe: dg@nhif.or.tz  
Tovuti: [www.nhif.or.tz](http://www.nhif.or.tz)  
Nukushi: +255-22-2133972,  
2133982



Makao Makuu,  
Tambukareli, Barabara ya Jakaya  
Kikwete,  
S.L.P. 1437, Dodoma,  
Tanzania

## TAARIFA KWA WATOA HUDUMA ZA MATIBABU KWA WANACHAMA WA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA NA WAAJIRI WANACHAMA KUHUSU UHAKIKI WA WATUMIAJI WA MIFUMO YA TEHAMA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA.

*Dodoma, Alhamisi, Juni 18, 2020:*

Katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wanachama na wadau wake, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unaendelea kufanya uhakiki wa watumiaji wa mifumo yake ya TEHAMA inayotumika katika utoaji wa huduma zake mbalimbali. Zoezi hili la uhakiki lilianza kutekelezwa tangu tarehe 10 Oktoba, 2019 kama ilivyotaarifiwa awali na linatarajiwa **kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2020.**

Kupitia zoezi hili, Watoa huduma na Waajiri wote wanaotumia huduma za NHIF wanatakiwa kujaza fomu maalum za uhakiki na kuorodhesha majina kamili kwa kila akaunti (user name) inayotumika kuingia katika mifumo mbalimbali ya NHIF wakati wa kupata au kutoa huduma pamoja na namba ya Kitambulisho cha Taifa (National ID Number). Fomu za uhakiki zinapatikana katika Ofisi ya NHIF katika mkoa husika na itarejeshwa katika ofisi hiyo.

Watoa huduma na Waajiri wanahimizwa kukamilisha zoezi hili kwa muda uliopangwa ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na kuzifunga akaunti zisizohakikiwa mara baada ya muda uliopangwa kwa zoezi hili kuisha.

NHIF inaendelea kuthamini ushirikiano na wadau wote na endepo kutahitajika maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Ofisi ya NHIF katika mkoa ulipo.

Imetolewa na;

Anjela Mziray

**MENEJA UHUSIANO**